

## Mwongozo wa Mpango wa Ushiriki wa Ndugu Vijana

Mwongozo huu unatoa mukhtasari wa Mpango, umuhimu wa ushiriki wa ndugu kwa ndugu, SO Wachezaji, Mipango na Olimpiki Maalum kwa jumla Pia inatoa mapendekezo mahsusi ya kuwezesha ushiriki wa ndugu katika Mipango ya Olimpiki Maalum.

### Haja ya Ushiriki wa Ndugu

Ndugu za watu walio na ulemavu wa akili (ID) wanaweza kupitia changamoto kama vile:

- 'Ulemavu kwa utengamano' kupitia kuchokozwa na kutengwa katika jamii;
- Kukosa uwezo wa kumudu shinikizo za familia, mara nyingi zinasababishwa na ID;
- Kuhisi kulemewa na majukumu ya kutunza; na
- Wasiwasi kuhusu jukumu lao katika kutunza hapo baadaye.

Ili kushughulikia changamoto hizi, Olimpiki Maalum inabuni mpango wa kushirikisha ndugu kwa usaidizi wa Samuel Family Foundation. Kupitia **misheni ya jumuisho**, ya Olimpiki Maalum, tunawezawapa ndugu za watu walio na ID:

1. Jamii inayowakubali;
2. Wenzao watakaowasaidia na watu wa kuigwa;
3. Nafasi za kuimarisha uhusiano kati yao na ndugu yao aliye na ulemavu wa kiakili; na
4. Fursa za kueleza waliyoyapitia na kukua kama viongozi maishani mwao.

Kwa hivyo, ndugu wanawezakuwa **viongozi wa vijana** walio na ufanisi katika harakati za Olimpiki Maalum kwa sababu wana:

1. Tajriba binafsi na ulemavu na kutengwa, inayowapa motisha imara ya utetezi;
2. Uhusiano wa maisha na mtu aliye na ulemavu wa akili, ambayo inapelekea ushiriki wa maisha; na
3. Ukaribu na Wachezaji wa SO, inayowafanya wawe rahisi kufikia kuliko vijana wengine.

Viongozi walio ndugu wamekuwa na watakuwa wa **muhimu** sana katika awamu na safu ya harakati za Olimpiki Maalum. Kwa mfano, mwanzilishi wa Olimpiki Maalum Eunice Kennedy Shriver alikuwa ndugu. Ndugu kama Soeren Palumbo wameendesha jitihada za utetezi kama vile kampeni ya R-word. Ndugu pia wamehusika kama Mjumbe wa Bodi, makocha, wajitoleaji, wafanyakazi na washiriki Walioungana.

### Je, Ushiriki wa Ndugu wa SO ni nini?

Ushiriki wa Ndugu wa SO hutokea ambapo ndugu wa mtu aliye na ulemavu wa akili anashiriki kikamilifu katika maisha ya ndugu ama dada yao aliye SO. Kwa pamoja, wanaweza kucheza, kusoma na kufanya kazi, wakiimarisha uhusiano wao katika hizo harakati. Ndugu hao ni timu ambayo wanapeana motisha na kusaidiana, badala ya kufanya kazi kibinafsi katika malengo yao binafsi. Katika muktadha wa Olimpiki Maalum, ushiriki wa ndugu unawezatokea katika nusra ya eneo au kikundi chochote. Harakati ya sasa ni maalum kwa ndugu kati ya miaka 8 hadi 25 na lengo kuwa wataendelea kushiriki na ndugu zao na Olimpiki Maalum katika utu uzima wote.

Mifano ya fursa za Olimpiki Maalum kwa ushiriki wa ndugu inajumuisha:

Aina ya Ushiriki	Fursa za Olimpiki Maalum
Kujitolea	Kujitolea kwa jumla, tukio la mara moja, Healthy Athletes®, kuendeleza
Kushiriki	Inclusive Young Athletes, Unified Sports®, ushiriki katika vyuo vikuu, kufunza
Afya na Uhodari	Unified Fitness Club, Fit Families, SOfit
Kuongana na Wengine	Mtandao wa Msaada wa Familia
Kutetea	Utetezi wa shule nzima na uongozi wa jumla kwa vijana
Uongozi wa Mipango	Wafanyakazi, Mkurugenzi wa Taifa, Mratibu wa Taifa wa Familia, kuongoza Kamati za Uamilisho za Vijana, kuongoza Mafunzo ya Uongozi wa Wanariadha, etc.

### Kuendeleza Ushiriki wa Ndugu

Zilizoorodheshwa hapo chini ni mikakati ya kuendeleza ushiriki wa Ndugu katika Nnji yako.

- Nufaika na juhudi za kusajili zilizomo kuhimiza ushiriki wa nduku.** Kwa mfano, wakati wa matukio ya kusajili wachezaji, wahimiza ndugu kujiandikisha kama washiriki Walioungana.
- Kutoa vifaa vinavyojumuisha ndugu kwa familia.** Unapogawa majarida, vipeperushi, machapisho ya mitandao ya kijamii, nk., tumia lugha inayoeleweka na kukaribisha ndugu kushiriki katika matukio ya Olimpiki Maalum na shughuli.
- Kutoa hadithi za ndugu.** Kusanya hadithi na mahojiano na ndugu na uzitoe kwa jamii yako. Kwa kutoa hadithi za ndugu katika Olimpiki Maalum, tunaweza kuwapa watu wengine motisha kushiriki, pia. Ruhusu ndugu kutumia sauti zao wanapotoa hadithi zao. Waulize jinsi Olimpiki Maalum imebadili uhusiano wao na ndugu zao na ni nini wangependa kuwaambia ndugu wengine ambao bado hawajihusishi na Olimpiki Maalum. Wasiliana na ofisi yako ya wilaya kwa habari zaidi kuhusu kukusanya na kutoa hadithi za ndugu.
- Fanya kazi na viongozi wa Mtandao wako wa Kusaidia Familia na/au Vikao vya Familia ili zijumuishe ndugu.** Fanya vikao vya ndugu, anzisha vikundi vya kuwasaidia, au uliza ndugu waongeleshe vikundi. Tumia Mtandao wa Kusaidia Familia kama njia ya ndugu kuungana na kupata jamii yao.
- Toa mkakati huu na makocha na Waratibu wa Mpango wa Eneo ambao wanafanya kazi moja kwa moja na wachezaji na familia.** Waulize watambue ndugu ambao wanaonyesha kutaka kushiriki zaidi na Olimpiki Maalum, na tena uwaunganishe na fursa zilizotajwa hapo juu.

### Rasilimali Saidizi

- [Mwongozo wa Mpango wa Ushiriki wa Ndugu Vijana](#)
- [Mwongozo wa Mzazi wa Mpango wa Ushiriki wa Ndugu Vijana](#)
- [Mwongozo wa Wachezaji wachanga katika Jamii na Nyumbani](#)
- [Unified Fitness Club, Fit Families](#) na [SOfit](#)
- [Story Starter Template](#) na [Medium Blog](#)

Kwa kushirikiana na



**Samuel Family  
Foundation**